

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA  
JAMII**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI KWA  
MWAKA 2018/2019**

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Idara ya Kamati za Bunge

S. L. P. 941,

**DODOMA.**

**7 FEBRUARI, 2019**

## YALIYOMO

<b>SEHEMU YA KWANZA</b> .....	1
<b>1.0 UTANGULIZI</b> .....	1
1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati .....	2
1.2 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati .....	3
<b>SEHEMU YA PILI</b> .....	4
<b>2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI</b> .....	4
2.1 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali .....	4
2.1.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto .....	4
2.1.2 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.....	15
2.1.3 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo .....	20
2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 .....	22
2.3 Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na wa Fedha wa 2017/2018 na mchakato wa Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 .....	24

2.4 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018).....	26
2.4.1 . Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto .....	27
2.4.2 .....Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo .....	37
2.4.3 ..... Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia .....	45
2.5 Kupokea Taarifa Mahsusni .....	51
2.5.1 . Taarifa ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhusu uanachama wa baadhi ya Taasisi za Serikali hususan Benki Kuu ya Tanzania (BOT).....	51
2.5.2 ..... <i>Taarifa kuhusu Visimbuzi</i> .....	53
2.7 Semina kwa Wajumbe wa Kamati .....	55
<b>SEHEMU YA TATU</b> .....	57
<b>3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI</b> .....	57
3.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Wizara ...	57
3.2 Miradi ya Maendeleo .....	58

3.3	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto .....	59
3.3.1	.....Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI) .....	59
3.3.2	..... Bajeti ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.....	61
3.3.3	..... Ukatili wa Kijinsia na Watoto .....	62
3.3.4	..... Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) .....	63
3.3.5	.....Bohari Kuu ya Dawa (MSD) .....	68
3.3.6	.....Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) .....	70
3.3.7	.....Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete .....	72
3.4	Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo .....	73
3.4.1	.....Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) .....	73
3.4.2	.....Sheria ya Huduma za Habari .....	74

3.4.3 .....	Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)	
.....		76
3.4.4 .....	TASUBA	
.....		78
3.4.5 .....	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	
.....		79
3.5	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia .....	81
3.5.1 .....	Mkakati wa kuboresha miundombinu ya Vyuu.....	82
3.5.2	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl J.K Nyerere kiendane na jina .....	83
3.5.3 .....	Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu .....	85
3.5.4	Miradi ya Lipa kulingana na Matokeo (EP4R) kusimamiwa na Wizara ya ELIMU .....	88
3.5.5 .....	Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) .....	89
3.5.6 .....	Vyuu vya Ufundi .....	90
3.5.7 .....	<i>Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)</i> .....	91
<b>SEHEMU YA NNE.....</b>		<b>93</b>

**4.0 HITIMISHO .....93**  
4.1 SHUKRANI .....93  
4.2 HOJA.....96

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA  
JAMII KWA MWAKA 2018/ 2019**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa mwaka 2018/ 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi wenye kueleza muundo na majukumu ya Kamati. Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo. Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na

Mapendekezo ya Kamati na mwisho kabisa ni Hitimsho la Taarifa.

## **1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii yameelezwa kwenye Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Aidha, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ambazo ni: -

- a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;



- b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
- c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

## **1.2 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/2019, Kamati imetekeleza shughuli mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kama ifuatavyo:

- a) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018;
- b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Wizara inazosisimamia;
- c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Taasisi za Wizara inazosisimamia;
- d) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018);
- e) Kuchambua Miswada ya Sheria; na
- f) Kushiriki Semina za mafunzo.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoielezwa awali, kwa mwaka 2018/2019 Kamati imetekeleza majukumu yake kwa kufanya uchambuzi na kujadili Taarifa mbalimbali pamoja na kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuchambua Muswada wa Sheria kama ifuatavyo:

#### 2.1 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, Katika nyakati tofauti kuanzia mwezi Machi, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara inazosisimamia kama ifuatavyo:-

##### 2.1.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliendelea kutekeleza majukumu mbalimbali uliyoipa yakiwemo kufuatilia utekelezaji wa

majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Taasisi ambazo Kamati ilikutana nazo na kuweza kupokea na kujadili Taarifa zao ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto (KDHI). Aidha, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa majukumu katika Hospitali za Mikoa nchini. Utendaji wa Taasisi hizo zilizotajwa ni kama ifuatavyo;

#### **a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 26 Oktoba, 2018 Waziri aliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yenye kujumuisha chimbuko la Mfuko huo pamoja na majukumu yake na ushirikiano wake na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma za Afya nchini. Mfuko huo ulianzishwa na kundi la watumishi wa Umma kwa kuzingatia dhana ya mshikamano wa kijamii katika

kuweza kugharamia huduma za afya miongoni mwa wanachama wake.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilieleza pia Mfuko wa Bima ya Afya una vyanzo vitatu vya mapato ambavyo ni pamoja na michango ya wanachama, mapato ya uwekezaji wa fedha katika miradi na vyanzo vingine mbalimbali. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, Mapato hayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 mapato yalikuwa ni shilingi **Bilioni 488.595** ambapo kwa mwaka 2018/2019 yanatarajiwa kuwa kiasi cha shilingi **Bilioni 589.283** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 17.0** ikilinganishwa na mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa pia kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo na ushauri mbalimbali wa Kamati ili kuboresha utendaji wa NHIF ikiwemo kubuni utaratibu wa kuwa na vifurushi vya Bima ya Afya ambavyo vitawawezesha wananchi wengi kupata huduma hiyo, kuyashawishi mashirika mbalimbali kujiunga na NHIF, kuhakikisha

Bima ya afya kwa wote (*Universal Health Coverage*) inaanza mapema, Mfuko kufanya re - insurance na makampuni mengine ya nje ili kusaidia kupunguza mzigo mkubwa kwa mfuko.

Mapendekezo yote haya yaliyotolewa na Kamati yetu na Serikali imekuwa ikiyafanyia kazi na hivyo kubuni vifurushi vipya vikiwemo **DUNDULIZA** na **JIPIMIE** ambavyo vinawanufaisha wananchi. **Kamati inapongeza jitihada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati ilielezwa baadhi ya mafanikio ambayo NHIF imepata hadi sasa ni kuongezeka kwa idadi ya wananchama wa Mfuko kutoka wanachama **164,708** mwaka 2001/2002 hadi kufikia wanachama **873,012** sawa na **asilimia 8** ya watanzania wote, Utekelezaji wa mpango wa Tumaini la Mama unaolenga kutoa bima ya afya kwa akina mama wajawazito, watoto na familia zao na kuwekeza katika miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo

ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa-Dodoma na Taasisi ya Mifupa MOI awamu ya tatu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo ya Mfuko, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zinazoendelea kuukabili Mfuko ikiwemo, kukosekana kwa uhiari wa wananchi kujiunga na Mfuko, kukosekana kwa huduma zinazolipiwa katika baadhi ya maeneo, watoa huduma kutotumia fursa ya mikopo itolewayo na Mfuko na kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanaongeza gharama kubwa kwa mfuko. **Kamati inaona kuwa kuna umuhimu na uharaka wa Serikali kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ili wananchi wengi waweze kujiunga na mfuko huu na kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote nchini kama zilivyo nchi za Ghana na Rwanda ambapo baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kwenda kujifunza na kuona huduma za afya zilivyoboreshwa kutokana na uwepo wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.**

**b) Bohari Kuu ya Dawa (Medical Stores Department - MSD)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Oktoba 2018, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bohari Kuu ya Dawa. Taarifa hiyo ilieleza Sheria inayompa mamlaka MSD kutekeleza majukumu yake (kifungu cha 3(2)). Aidha, kifungu cha 4 (2) cha Sheria ya MSD kinaeleza majukumu makuu ya MSD ambayo ni pamoja na kutengeneza, kusimamia na kuendesha mfumo wa kibiashara wenye tija ya manunuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa, MSD inahudumia jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo **5,432** nchi nzima kupitia Bohari za Kanda nane (8) ambazo ni Kanda ya Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Iringa, Dodoma, Tabora, Mwanza na Moshi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa baadhi ya mafanikio ambayo MSD imepata hadi sasa ambayo ni pamoja na ufikishaji wa dawa katika maeneo mengi ya nchi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuingia mikataba ya ununuzi wa dawa na wazalishaji moja kwa moja bila kupitia kwa mtu wa kati na kufanikisha kushusha bei baadhi ya dawa na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa dawa muhimu hadi kufikia **asilimia 93** nchi nzima kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa MSD inasambaza dawa zenye thamani ya shilingi **Bilioni 600** kwa Mwaka kwa nchi nzima. Aidha, kuhusu kuanzishwa kwa mradi wa uzalishaji wa dawa kwa ushirikiano na Sekta binafsi, Waziri alieleza mchakato wake unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka huu 2019 ambao utawezesha kukuza uchumi wa nchi na kuongeza upatikanaji wa dawa kwa wakati. **Ni Imani ya Kamati kuwa mradi huu utaanza kama ambavyo Waziri aliieleza na**



**kutatua changamoto zitokanazo na uagizaji wa dawa nje ya nchi.**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto kubwa ambayo MSD inakabiliwa nayo ya mtaji mdogo wa kununua dawa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za kununua dawa kutoka katika vituo vya kutolea huduma ya afya na kuongezeka kwa deni la Serikali linalofikia shilingi **Bilioni 200** ambazo linachangiwa na ununuzi wa Dawa na usambazaji wake. **Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha deni hili linalipwa mapema ili MSD iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.**

**c) Idara Kuu Maendeleo ya Jamii kuhusu Asasi zisizo za Kiserikali (AZAKI)**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI) iliwasilishwa katika kikao kilichofanyika Mwezi Oktoba, 2018. Kamati ilielezwa kuhusu chimbuko la Asasi hizo, Sera inayoongoza

AZAKI ya mwaka 2001 na Sheria yake ya mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa pia utaratibu wa usajili wa AZAKI ambao unafanyika katika Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Viwanda na Biashara jambo ambalo Kamati inaona linaleta mkanganyiko.

**Mheshimiwa Spika**, AZAKI zimekuwa zikitekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kama vile kuwezesha shughuli mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Maji na Elimu katika ujenzi wa majengo na uhamasishaji wa jamii kubadili tabia, ujenzi wa miundombinu ya maji, miundombinu ya elimu na kutoa huduma kwa makundi maalumu wakiwemo watoto, wazee na wasiojiweza. Aidha, AZAKI zinatoa fursa za ajira kwa watanzania wapatao **3414** hadi kufikia 2015 na kuongezeka kwa mapato kila mwaka yatokanayo na fedha za ada na faini za Asasi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mchango wa AZAKI kwa jamii ya Watanzania kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara katika kuratibu shughuli za AZAKI. Changamoto hizo ni pamoja na kutegemea fedha za wafadhili zenye masharti magumu, Mashirika mengi kufanya shughuli zake katika maeneo ya mjini, kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa AZAKI na Wataalamu kutotumika katika upangaji na utekelezaji wa shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na changamoto hizo, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na kuimarisha Sheria ya AZAKI, kufanya mapitio ya Sera ya AZAKI na kuimarisha ushirikiano na vyombo vya dola jambo ambalo ni jema.

**d) Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto (KDIH)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 31 Agosti, 2018, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Hospitali ya

Magonjwa ambukizi Kibong'oto ambayo ilianzishwa Mwaka 1926 katika Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kutoa huduma za Kifua Kikuu (TB). Mwaka 2010 Hospitali hiyo ilitangazwa kupitia gazeti la Serikali Namba 828 kuwa ni Hospitali maalumu ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi (*Kibong'oto Infectious Disease Hospital*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa Majukumu makuu ya Hospitali ni pamoja na kufanya uchunguzi, tiba na ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza hasa TB, UKIMWI na Magonjwa ya Mapafu yasiyoambukiza, kutoa Mafunzo na tafiti kwa changamoto mbalimbali za afya hasa magonjwa ambukizi na mapafu yasiyoambukiza pamoja na kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya mlipuko na magonjwa yale ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa pamoja na hospitali hiyo kuwa Maalum Kitaifa kwa Magonjwa Ambukizi lakini haifahamiki kwa wananchi wengi. **Kamati inaona hali hii inaweza**

**kufanya mapambano dhidi ya kifua kikuu kutofanikiwa mapema.**

## **2.1.2Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kupokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Taasisi mbalimbali zikiwemo Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kama ifuatavyo: -

### **a)Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 31 Oktoba, 2018 Wizara iliwasilisha Taarifa ya utendaji wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa-iringa. Chuo hicho ambacho awali ilikuwa ni Shule ya Sekondari Mkwawa kilianzishwa rasmi tarehe 1 Septemba, 2005 kama sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam. Chuo kinatoa Shahada za awali ambazo ni Shahada ya Elimu ya Jamii na Ualimu (B.A. Ed), Shahada ya Elimu katika Elimu ya Jamii (B. A Ed. Arts), Shahada ya Elimu

katika Sayansi (B.Ed.-Sc) na Shahada ya Sayansi na Ualimu (B. Sc – Ed). Aidha, Chuo kinatoa Shahada ya Uzamili/Umahiri ya Elimu (*Postgraduates Diploma in Education*) na Shahada za Umahiri/Uzamili za Sayansi na Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa juu ya Miradi ya Maendeleo ambayo inatekelezwa na Chuo. Miradi hiyo ni pamoja na:-

- i) Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1009 na ujenzi wake ulianza mwaka 2008 kwa sasa umekamilika kwa **asilimia 91** na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, mwaka huu 2019. Gharama za mradi ni shilingi **8,803,763,551.97**;
- ii) Mradi wa Ujenzi wa Maabara za Sayansi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 270 kwa wakati mmoja kwa gharama ya shilingi **2,153,127,897.14**;
- iii) Ujenzi wa Ofisi za Wahadhiri 20 zenye uwezo wa kuchukua wahadhiri 40 kwa gharama ya

shilingi **323,833,786.27** ambao umekamilika tangu tarehe 28 Agosti, 2018;

- iv) Mradi wa Uchimbaji wa Kisima cha maji ambao ulianza Septemba 2017 na kukamilika Novemba 2017 kwa gharama ya shilingi **103,990,000**. Kisima kimoja kina uwezo wa kuzalisha lita za ujazo 3000 kwa saa na Chuo kinaendelea kukamilisha uwekaji wa miundombinu kama mabomba, ujenzi wa matenki na ufungaji wa pampu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi inayoendelea chuoni hapo, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto ambazo chuo inakumbana ambazo ni kutowajibika kikamilifu kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Jengo la Mihadhara hali inayochelewesha ukamilikaji wa mradi na upungufu wa miundombinu (Kumbi za mihadhara, ofisi za wahadhiri, maktaba na mabweni). **Kamati inaona ni vyema sheria ikachukua mkondo wake hasa kwa mkandarasi ambaye ameshindwa kutimiza wajibu wake.**

## **b) Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere mnamo tarehe 1 Novemba, 2018. Taarifa ya Chuo ilieleza kuhusu Chimbuko la chuo ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 29 Julai, 1961. Aidha, kuanzia Mwaka 1971 hadi 1992 Chuo hicho kilijulikana kama Chuo cha Chama na kuanzia 1992 hadi 2005 kilikuwa kikijulikana kama Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni na mnamo tarehe 01 Oktoba, 2005 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu kilianzishwa rasmi chini ya Sheria ya Bunge Na. 6 ya Mwaka 2005.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, chuo kina majukumu mbalimbali yakiwemo ya utoaji mafunzo katika fani za Sayansi Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada, kutoa mafunzo ya Uongozi (*Leadership*), kuendesha mafunzo ya Elimu ya kujiendeleza na kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta za umma na binafsi.



**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa malengo kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi sasa, Kamati ililezwa kuwa, chuo kimefanya kazi mbalimbali licha ya changamoto ya fedha hususan fedha za Miradi ya Maendeleo. Malengo yaliyotekelezwa na chuo kwa kipindi hicho ni pamoja na;

- i) Kuinua ubora wa Elimu na mafunzo katika taasisi kwa kuboresha mazingira kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kufundishia;
- ii) Kugharamia uandaaji wa mitaala na ununuzi wa samani na vifaa mbalimbali; na
- iii) Kumalizia ujenzi wa Jengo la Hosteli Kampasi ya Kivukoni na Ukumbi wa Mihadhara na kuongeza udahili kwa wanafunzi wapya 2900.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo hayo yaliyotekelezwa na Chuo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto kuu tatu zinazokikumba Chuo kuwa ni uchakavu wa miundombinu (nyumba za watumishi, majengo na barabara), uhaba wa Ofisi za Watumishi na madarasa ya kufundishia na uhaba wa hosteli za wanafunzi katika Kampasi ya

Zanzibar kwani hakuna hosteli katika eneo la chuo jambo ambalo Kamati inaona linaathiri maendeleo na upanuzi wa chuo.

### **2.1.3Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi mbili zilizo chini ya usimamizi wa Wizara hii.

#### **a)Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa kuhusu utendaji wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) iliwasilishwa na kujadiliwa na Kamati mnamo tarehe 29 Oktoba, 2018. BAKITA ambayo imeanzishwa mwaka 1967 kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ni chombo cha Serikali katika kusimamia maendeleo na matumizi ya Kiswahili kitaifa na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, BAKITA ina jukumu la ukuzaji na usambazaji wa misamiati na istiahi, usimamiaji wa matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili, utoaji na uimarishaji huduma ya tafsiri na ukalimani na uandaaji wa mazingira wezeshi kwa ajili ya kubidhaisha Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu hayo, Kamati ilielezwa kuhusu masuala mbalimbali kama vile Kanzidata (*Database*) kwa ajili ya kusajili na kutunza kumbukumbu za Wataalamu wa Kiswahili imeanzishwa na hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 tayari wataalamu wa kiswahili 270 wamesajiliwa, Mradi wa kuunda Kongoo ya Kiswahili umeanza kutekelezwa; na Baraza limeanza kuandaa machapisho yatakayosaidia kuendeleza Kiswahili Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa baadhi ya changamoto ambazo BAKITA inakumbana nazo ikiwa ni pamoja na;

- i) Kutokuwa na Mamlaka ya Kisheria ya kutoa adhabu kwa wanaokiuka maelekezo na matamko mbalimbali ya Serikali kuhusu matumizi na Maendeleo ya Kiswahili;
- ii) Kutotumika kwa lugha ya kiswahili katika Elimu jambo linalofanya istilahi zilizoundwa na kuratibiwa na Baraza kubaki katika mashubaka;
- iii) Baadhi ya nyaraka za Serikali kutopitishwa BAKITA kwa ajili ya kuthibitisha lugha;

iv)Ufinyu wa Bajeti unaokwamisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Taasisi na Uhaba wa Watumishi. Kamati inatambua kuwa bajeti ya Taasisi imekuwa ikitegemea ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani. Hata hivyo, imebainika kuwa kuanzia mwaka 2014 – 2018 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo licha ya kuwa Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha fedha hizo. **Kamati imesikitishwa sana na hali hii.**

## **2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inazipa majukumu Kamati za Kudumu za Kisekta ikiwemo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya jamii kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2017/2018) iliyo chini ya Wizara zinazozisimamiwa na Kamati.


**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza kanuni hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea jumla ya miradi mitano (5) iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 iliyokuwa inatekelezwa katika mkoa wa Iringa na Mbeya. Miradi hiyo ni pamoja na;

- a) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Rungemba, Mufindi -Iringa **(Namba ya Mradi 6330)**;
- b) Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Uyole **(Namba ya Mradi 6330)**;
- c) Mradi wa Hospitali ya Kanda Mbeya **(Namba ya Mradi 5422)**;
- d) Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa **(Namba ya Mradi – 4314)** ; na
- e) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya **(Namba ya Mradi 6333)**.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inatembelea na kukagua Miradi hiyo, hakuna hata mradi mmoja uliokuwa umepelekewa fedha licha ya fedha kuidihinishwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha shilingi **Bilioni 6.832** kama

ilivyoelezwa kwenye Taarifa ambayo Kamati iliwasilisha mwezi Mei, 2018 wakati wa uchambuzi wa Bajeti. Hali ya upatikanaji wa fedha ni kama ambavyo imeoneshwa katika Kielelezo Na.1

**Kielelezo Na.1: Hali ya upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo 2017/2018**



**Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

### **2.3 Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na wa Fedha wa 2017/2018 na mchakato wa Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilikutana katika vikao vyake na Wizara inazozisimamia kwa

ajili ya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika vikao vya uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Taarifa juu ya utekelezaji huo ziliwasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ambayo Kamati ilikuwa imeyatoa kwa Wizara inazosisimamia ulikuwa unategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha. Kama ambavyo imeelezwa awali, hali ya upatikanaji wa fedha imekuwa ni changamoto inazozikabili Wizara zote na hivyo kuathiri utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo mengi ya Kamati. Baadhi ya Maoni ambayo Kamati inaona ni ya msingi na bado mpaka sasa hayajatekelezwa ipasavyo ni pamoja na:-

- Tuzo ya Udhamini (*Scholarship Award*) hasa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya kidato cha sita ambayo Kamati ilipendekeza iitwe *Magufuli Scholarship Award*;

- Uainishaji wa Vyuo Vikuu (*University Classification*) kulingana na ubora wake kutokana na kuendelea kuibuka kwa vyuo vingi hapa nchini;
- Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote (*Universal Health Coverage Bill*) kuletwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaisisitiza na kuendelea kuishauri Serikali maeneo haya na yale yote iliyoyapendekeza katika Taarifa zake za awali iyafanyie kazi.**

#### **2.4 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018)**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha tarehe 14 hadi 25 Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa majukumu na Bajeti za Wizara na Taasisi inazosisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2018) kama ifuatavyo:-



## 2.4.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto


**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 Januari, 2019, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliwasilisha Taarifa yake ya utekelezaji wa majukumu na Bajeti za Wizara na Taasisi inazosisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba,2018) ambayo ilipokelewa, kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Katika Taarifa hiyo Wizara ilieleza majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa, na **Fungu 52 (Idara Kuu Afya)**, baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na Mpango wa Taifa wa chanjo umefikia asilimia 97, Afya ya Uzazi na Mtoto imefikiwa kwa **asilimia 59** ikilinganishwa na **asilimia 48** mwaka 2017, upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba hususan dawa muhimu katika vituo vya afya umefikia asilimia 96.7, pamoja na chupa za damu salama zilizokusanywa ni 158,755 kati ya 375,000 zilizopangwa sawa na **asilimia 42.3** ya lengo. **Kamati inapongeza jitihada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, ukusanyaji wa maduhuli umetekelezwa kwa **asilimia 52 (153,520,009,883/= kati ya 297,013,657,702/=** zilizokadiriwa). **Kamati inaipongeza**

**Wizara kwa ukusanyaji huu mzuri wa maduhuli na ni matumaini ya Kamati kuwa ukusanyaji utafika asilimia 100 ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.**

Aidha kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwa Fungu 52, Kamati inaona hali siyo nzuri kwani ni **asilimia 27** tu ya fedha ndiyo zimepokelewa hadi kufikia Disemba, 2018 kama inavyooneshwa katika kielelezo Na. 2.

**Kielelezo Na. 2: Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 52)**




**Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)**, Wizara ilieleza majukumu yaliyotekelezwa kuwa ni pamoja na kusimamia utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii ambapo wanafunzi 2,677 wamedahiliwa hadi kufikia Disemba, 2018 vikundi vya malezi 1,184 kwenye Halmashauri 15 vimeanzishwa ili kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, wazee wasiojiweza 247,771 wamepata vitambulisho vya matibabu na jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 518 yamesajiliwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Taarifa hiyo ya utekelezaji wa majukumu, Kamati ilielezwa katika **Fungu 53** ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia Disemba 2018 ulikuwa ni shilingi **1,172,961,441/=** kati ya **3,090,796,000/=** sawa na **asilimia 37.9**. **Kamati inashauri Wizara iongeze jitihada za ukusanyaji wa maduhuli**. Aidha, upatikanaji wa fedha hadi kufikia Disemba 2018 ni **asilimia 39.7** kama inavyoonekana katika kielelezo Na.3

**Kielelezo Na.3 : Hali ya upatikanaji wa Fedha kwa Bajeti ya 2018/2019  
(Fungu 53)**



**Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

**a) Hospitali ya Taifa Muhimbili**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vyake vya mwezi Januari, 2019. Kamati ilipokea na kujadili Tarifa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambayo imeanzishwa kwa Sheria Na. 5 ya Bunge ya Mwaka 2000 ikiwa ni Mrithi wa lililokuwa Shirika la Afya Muhimbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2018/2019 kazi mbalimbali zilipangwa na zimetetelezwa. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na

kutoa na kuboresha huduma za kibingwa ambapo wagonjwa 274,776 wameonwa, kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa 159,663 wakiwemo 30,189 wa magonjwa ya dharura, upasuaji kwa wagonjwa 8,747 umefanyika, wagonjwa 31,206 wamepata huduma za radiliojia (*CT-Scan, Ultrasound* na *MRI*), Wagonjwa 19 wamepata huduma ya kupandikizwa figo hali iliyosadia pia kuokoa gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi pamoja na kukamilisha kazi ya uboreshaji wa jengo la upasuaji kutoka vyumba 13 hadi 19.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha nusu mwaka, Hospitali imepata **asilimia 73.3** ya bajeti (**59,038,846,864/=** kati ya **87,141,998,341/=**). **Kwa mwenendo huu Kamati ina amini lengo litafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka.**

#### **b) Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) katika vikao vyake vya Mwezi

Januari, 2019. Taasisi ambayo ni Maalum kwa tiba ya magonjwa ya moyo imeanzishwa Septemba, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018, JKCI ilipanga na kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuajiri Watumishi 10, wagonjwa 44,250 walihudumiwa, upasuaji wa wagonjwa 211 ulifanyika, upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo (*catheterization laboratory*) ulifanyika kwa wagonjwa 521, wodi mpya ya watoto imeanzishwa ikiwa na vitanda 32 pamoja kufanya kambi 20 sehemu mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Taasisi nyingine na Mashirika mbalimbali duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa hali ya bajeti siyo mbaya kwani hadi kufikia Disemba, 2018, JKCI imepata shilingi **11,942,393,915/=** kati ya **22,911,630,045/=** sawa na **asilimia 52.1** ya bajeti. **Kamati inashauri jitihada hizi ziendelee.**

### c) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) katika vikao vya mwezi Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Nusu Mwaka MOI imefanikiwa kutoa matibabu kwa wagonjwa 102,820 wakiwemo wa wagonjwa wa upasuaji 3,024; kuimaridha upasuaji wa mgongo kwa tundu dogo (minimum invasive spine surgery) baada ya kununua darubini ya kisasa na seti maalum ya kufanyia upasuaji huo; wagonjwa 55,920 walipatiwa huduma za tiba mazoezi (*phisotherapy*) ikilinganishwa na wagonjwa 44,568 wa Disemba 2017 ongezeko la **asilimia 20. Kamati inapongeza jitihada hizi**. Aidha, kuhusu upatikanaji wa damu salama, jumla ya chupa 3911 zilikusanywa kati ya hizo chupa 3698 (94.5%) zilikuwa salama na 213 hazikuwa salama.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu suala la bajeti, kiasi kilichopatikana ni shilingi **9,292,847,124/=** kati **16,923,352,451/=** sawa na **asilimia 54.9. Kamati**

**inapongeza Serikali kwa utoaji mzuri wa fedha na inashauri utaratibu huu mzuri uendelee.**

#### **d)Mamlaka ya Chakula na Dawa**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 17 Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Mamlaka hiyo ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 na inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali , Sura 245 na Marekebisho yake ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, Katika wasilisho hilo, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2018, Mamlaka imetekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kusajili maeneo na kutoa vibali vya biashara ya chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambapo maombi 3281 ya usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vipodozi na vifaa yalipokelewa na kati ya hayo maombi **3203** sawa na **asilimia 98** ya maombi yaliidhinishwa, imeteketeza bidhaa zisizokidhi ubora na usalama wa mlaji ambapo jumla ya tani **453.6**



za bidhaa zenye thamani ya shilingi **Bilioni 6.94** ziliteteketewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji wa majukumu, Kamati pia ilielezwa kuhusu utekelezaji wa bajeti ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa ni shilingi **22,071,294,712** sawa na **asilimia 41** ya lengo la kukusanya **53,310,168** kwa Mwaka, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara umekuwa ni **asilimia 12 (1,446,740,275/=)** ya kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi **6,745,600,534/=**. **Kamati imesikitishwa na hali hii.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto ambazo Mamlaka inakumbana nazo na mbinu za kukabiliana nazo ikiwemo changamoto ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 kupitwa na wakati na hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya sasa ya udhibiti ambapo maandalizi ya mapendekezo ya mapitio ya Sheria kwaajili ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuridhia umekamilika. **Kamati inaitaka Wizara kuharakisha kuleta mapendekezo ya marekebisho hayo ili Bunge liweze**

**kufanyia kazi na hatimaye kuwa na sheria yenye tija na inayoendana na wakati.**

**e) Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 26 ya Mwaka 1973 kwa lengo la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na ushauri weledi katika maeneo ya ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na taaluma zinazoshabihiana na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 yakiwemo:-

- i) Kutoa mafunzo bora ya kitaaluma ambapo wanafunzi **1,064** walidahiliwa ikilinganishwa na **1,185** ya mwaka 2017/2018;
- ii) Kuimarisha mifumo ya tafiti, ushauri weledi na mafunzo ya muda mfupi ambapo Tafiti mbili zinazohusu masuala ya ustawi wa jamii zimefadhiliwa na chuo; na
- iii) Kuwezesha utawala bora na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ambayo yametokelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mwenendo wa Bajeti, Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Taasisi ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **10,403,984,423/=**. Hadi kufikia Disemba 2018, makusanyo yalikuwa ni **2,900,920,291/=** sawa na **asilimia 27.8 tu** ya Bajeti. Aidha, kwa upande wa upatikanaji wa fedha za Mishahara kutoka Serikalini, Taasisi ilipokea kiasi cha shilingi **1,476,990,000/=** sawa na asilimia **29.2** ya kiasi cha shilingi **5,054,574,423/=** kilichoidhinishwa na Bunge. **Kamati inaona kwamba kwa mwenendo huu ni vigumu kufikia malengo na hivyo kuitaka Taasisi kuongeza juhudi za makusanyo ya maduhuli lakini pia Serikali kuhakikisha inaipatia fedha Taasisi hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge.**

#### **2.4.2Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**


**Mheshimiwa Spika**, kikao cha kujadili Taarifa ya Wizara hii kilifanyika tarehe 18 Januari, 2019. Katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018 Wizara ilipanga kutekeleza kazi mbalimbali. Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2018, Wizara iliratibu vipindi 17 vyenye kuelimisha Umma, Magazeti mapya 7 yalisajiliwa na leseni za magazeti 59 zilihuishwa pamoja na

vitambulisho (*press cards*) 54 vilitolewa kwa Waaandishi wa Habari. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenye umri chini ya miaka 17 (AFCON U -17) yatakayofanyika mwezi April, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na taarifa hiyo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati ilielezwa ukusanyaji wa maduhuli ambapo ilikadiriwa kiasi cha shilingi **1,077,804,000/=**. Hadi kufikia Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya **516,548,949/=** sawa na **asilimia 47.9** ya lengo. **Kamati inaipongeza Wizara na inashauri jitihada ziendelee ili kufikilia lengo la mwaka.**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa fedha ni **asilimia 48** kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.4.

## Kielelezo Na.4: Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 96)



### **Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

#### **a) Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TASUBA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TASUBA) katika vikao vya Mwezi Januari, 2019. Taasisi hii ambayo ni Wakala wa Serikali ilianzishwa Mwaka 1997 na

ilitokana na kilichokuwa Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

**Mheshimiwa Spika**, TASUBA ni moja kati ya Taasisi tatu zilizoteuliwa kuwa kituo chenye ubora uliotukuka (*Centre of Excellence*) ili kuendesha mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa Wasanii wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kukuza Sanaa na utafiti kwenye eneo la utamaduni pamoja na kuratibu na kuendesha Tamasha la Sanaa na Utamaduni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018) TASUBA ilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya kufundisha wanachuo 249 kwa kozi mbalimbali, kuendesha Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo mnamo mwezi Oktoba 2018 lililohudhuriwa na watu wapatao 58,000 na vikundi 89 vikiwemo kutoka Kenya, Finland, Ujerumani na Zimbabwe.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bajeti, Kamati ilielezwa kwa kipindi cha nusu Mwaka imefanikiwa kukusanya maduhuli ya shilingi **249,472,100/=** sawa na **asilimia 58.4** ya kiasi cha shilingi **427,000,000/=** kilichopangwa kukusanywa kwa Mwaka. Kwa upande wa mishahara, kiasi kilichopokelewa ni **488,045,000/=** sawa na **asilimia 30.7** ya kiasi cha shilingi **1,589,232,000/=** kilichopangwa. Aidha, kuhusu Fedha za matumizi mengineyo (OC) jumla ya shilingi **9,670,000/=** zilipokelewa kati ya **23,213,000/=** zilizopangwa sawa na **asilimia 41.6**. Hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. **Kamati imesikitishwa kuona pamoja na umuhimu wake bado Taasisi hii haitengewi fedha za kutosha na hata za miaka ya nyuma hususan za miradi ya maendeleo mpaka sasa hazijatolewa licha ya ushauri wa Kamati wa mara kwa mara.**

**b) Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 Januari, 2019 Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya

utekelezaji wa majukumu na bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka. TBC ambayo imeanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 186 la Mwaka 2007 ina jukumu la kutoa habari mbalimbali kwa umma, kuburudisha na kuelimisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, TBC ilipanga kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Dodoma ambapo Michoro ya Jengo imekamilika na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa TBC, ukarabati wa Studio za Redio na Televisheni Makao Makuu – Dodoma ambao unaendelea, kuanzisha chaneli ya Utalii ambayo ilizinduliwa na Waziri Mkuu tarehe 15 Disemba, 2018, ununuzi wa magari 11 na kibali chake kimeshatoka pamoja na kukamilisha miradi ya usikivu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha yenye kuonesha ukusanyaji wa maduhuli umekuwa ni shilingi **3,300,960,057/=**



kati ya shilingi **11,940,540,000/=** zilizopangwa sawa na **asilimia 27.6** tu. Aidha, kuhusu Mishahara, TBC ilipokea shilingi **4,478,125,720/=** sawa na asilimia **56.4** ya kiasi cha shilingi **7,928,824,000/=** zilizoidhinishwa na Matumizi mengineyo **asilimia 31.6 (1,330,000,000/=)** kilipokelewa kati ya **4,200,000,000/=** kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi **2,500,000,000/=** sawa na **asilimia 50** ya shilingi **5,000,000,000/=** kilichotengwa kimepokelewa. **Kamati inashauri fedha hizi ziendeleo kutolewa ili ifikapo mwisho wa mwaka, fedha zote ziwe zimetolewa.**

**c) Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) katika vikao vyake vya mwezi Januari, 2019. BASATA ilianzishwa kwa Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 ambayo pia ilielezwa kuwa imepitwa na wakati.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018 BASATA imetekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo kufanya usajili wa wasanii na wadau 845 nchini, kuendesha mafunzo kwa viongozi wa vyama na vikundi vya wasanii na wadau wa Sanaa wapatao 60, midahalo 29 ya jukwaa la Sanaa katika mikoa 13 ya Tanzania Bara iliendeshwa, jumla ya kazi za muziki zipatazo 256 zilihakikiwa na kupewa idhini ya kutumika katika jamii, vikao na Maafisa Utamaduni 152 katika Halmashauri 51 vimefanyika na kufanya vikao vya kujenga uelewa juu ya Kanuni Na. 43 za Mwaka 2018 kwa wasanii na wadau wa Sanaa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla bajeti iliyopokelewa ni **asilimia 45** ya fedha iliyoidhinishwa (**457,954,250/=** kati ya **1,012,277,000/=**) ikiwa na mchanganuo wa Maduhuli yaliyokusanywa kiasi cha shilingi **190,858,250/=** kati ya shilingi **478,080,000/=** zilizopangwa kukusanywa sawa na **asilimia 39.9**.

Fedha za Mishahara zilizopokelewa ni shilingi **255,492,000/=** sawa na **asilimia 50** ya shilingi **510,984,000/=** zilizoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa matumizi mengineyo (OC) kiasi cha shilingi **11,604,000/=** sawa na **asilimia 49.9** cha shilingi **23,213,000/=** kilichotengwa kilipokelewa. Kama ilivyokuwa kwa TASUBA, **hakuna fedha iliyotengwa kwaajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.**


#### **2.4.3Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara hii pamoja na taasisi zake mnamo tarehe 22 Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuhusu majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Wizara kwa kipindi cha Nusu Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kusimamia lthibati na uthibiti shule ambapo jumla ya shule 163 zimesajiliwa zikiwemo shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu na kubaini upungufu wa walimu katika shule za msingi na uhaba wa miundombinu kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi (Elimu bila malipo).

Aidha, Asasi 11,327 zimekaguliwa, Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi vimewekewa samani, Wizara imeandaa na kuzindua Mwongozo wa kutambua na kuendeleza ugunduzi, ubunifu na maarifa pamoja na kuanza Ujenzi wa Ofisi ya Wizara Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa Bajeti, ukusanyaji wa maduhuli umefanyika kwa **asilimia 47 (216,582,868,016/=** kati ya **460,011,442,840/=)**. Aidha, kuhusu upatikanaji wa fedha, hadi kufikia Disemba 2018 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 43.9** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 5.

**Kielelezo Na. 5 Hali ya upatikanaji wa fedha kwa  
Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 46)**



### ***Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ni imani ya Kamati kuwa hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 mafanikio yatakuwa zaidi ya asilimia 90.**

#### **a) Chuo Kikuu cha Dodoma;**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa

majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Chuo ikiwa ni pamoja na kudahili wanafunzi 11,854 sawa na asilimia 96.6 ya lengo la kudahili wanafunzi 12,269, kufanya tafiti 2, kutoa huduma za ushauri elekezi 11, kuboresha mahusiano (*collaborations*) na Taasisi 53 za Kitaifa na Kimataifa, kununua magari 8 kati ya 10 yaliyopangwa kununuliwa na kukarabati majengo ya Chuo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bajeti, Kamati ilielezwa kuwa Chuo hakijatengewa fedha za maendeleo hali inayoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwemo wa ukamilishaji wa ujenzi wa chuo ili kufikia lengo la kudahili wanafunzi 40,000. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto ya uhaba wa watumishi ambapo mahitaji halisi ni watumishi 2066 lakini waliopo ni watumishi 1436 sawa na **asilimia 69.5** tu ya lengo. **Kamati inaona kuna umuhimu wa kuongeza idadi ya watumishi kwa Chuo hiki.**

**b) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa kipindi cha nusu mwaka. Katika taarifa hiyo, mambo kadhaa yalibainika ikiwemo:- wanafunzi 40,114 walipatiwa mikopo kati ya wanafunzi 57,000 waliokuwa na vigezo kutokana na ufinyu wa bajeti, ukusanyaji wa mikopo umefikia **Bilioni 94**, wanufaika wapya 12,612 wamebainiwa na kuongeza idadi ya wanaolipa mikopo kufikia 207,319. Aidha, kuhusu ukusanyaji wa mikopo, hadi kufikia Disemba, 2018 Bodi ilikusanya **asilimia 63** ya lengo **(492,226,037,371/= kati ya 784,020,977,577/=)**.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu upatikanaji wa bajeti, Bodi imepokea **240,829,473,494/=** kati ya **427,554,000,000/=** sawa na **asilimia 56.3** ya lengo. **Kamati inapongeza Serikali kwa utoaji huu mzuri wa fedha hali ambayo inasaidia wanafunzi kupata mikopo kwa wakati, ni maoni ya Kamati kwa Serikali kuongeza fedha kwa bodi ya Mikopo ili kuweza kuwalipia wahitaji waliobaki.**

**c) Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kipindi cha nusu mwaka katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa majukumu ambayo Tume ilipanga kuyatekeleza na namna ilivyoyatekeleza, baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya utafiti zikiwemo Maabara za utafiti wa Taasisi za Utafiti wa Mifugo Tanga, Uyole na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa TAFIRI Musoma, kufadhili miradi 10 ya utafiti katika maeneo ya vipaumbele vya Taifa ikiwemo Viwanda, kusambaza matokeo ya utafiti ambapo vipindi na makala 42 yaliandaliwa na kusambazwa katika Redio na Televisheni.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na utekelezaji huo wa majukumu, Kamati ilichambua hali ya upatikanaji wa fedha ambapo ilibainika kuwa kwa ujumla Tume



imepokea **asilimia 53** ya bajeti yake (**15,475,438,936/=** kati ya **29,468,130,633/=**). **Kamati inapongeza jitihada hizi ingawa bado fedha hizi zinazoidhinishwa ni kidogo na haziendani na majukumu makubwa ya Taasisi hii. Aidha, Kamati imesikitishwa na Taasisi hii muhimu kuondolewa chanzo chake kingine cha fedha zitokanazo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (*Tele-Traffic Monitoring System*).**

## **2.5 Kupokea Taarifa Mahsusi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa mahsusi mbili kama ifuatavyo:-

### **2.5.1 Taarifa ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhusu**

**uanachama wa baadhi ya Taasisi za Serikali hususan Benki Kuu ya Tanzania (BOT)**

**Mheshimiwa Spika, Kamati** ilipata fursa ya kufuatilia suala la uanachama wa baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania. Itakumbukwa kuwa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura ya 395, inataka Watumishi wote wa Umma kuandikishwa na kunufaika na huduma zitolewazo na Mfuko huu kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei 2018, watumishi wengi walikuwa tayari wamejiunga kwa zaidi ya **asilimia 99** kama ilivyo katika Sheria wakiwemo Watumishi kutoka Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika ya Umma isipokuwa Benki Kuu ambayo ni Taasisi ya Serikali. Benki Kuu ilikuwa inataka huduma za ziada ambazo zilipaswa kulipiwa kwa malipo ya ziada. Kwa maelezo ya Wizara ni kuwa kama Benki Kuu wangejiunga na NHIF gharama yao ingekuwa kiasi cha shilingi **3,466,768,226/= (Premium)** kwa mwaka kwa huduma za kawaida kama watumishi wa taasisi nyingine. Lakini kwa kuwa Benki Kuu ilikuwa na mahitaji maalum kwa maana ya kuhitaji huduma za ziada jumla ya Shilingi **1,838,439,986/=** zingehitajika kwa ajili ya kupata huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilitoa ushauri mzuri ambao ulifanyiwa kazi na Serikali na suala hili la BOT kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) limefanikiwa na kwa sasa BOT ni wanachama wa NHIF.

## 2.5.2 Taarifa kuhusu Visimbuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya mwezi Agosti, 2018 Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wanaomiliki vyombo vya habari na wale wanaotoa huduma ya habari kupitia visimbuzi wakiwemo Startmedia, ZUKU, AZAM Media kwa ajili ya kujadili kusitishwa kwa urushaji wa maadhui kupitia baadhi ya vituo vya ndani ya nchi (*local channels*) vya kurushia matangazo kufuatia tamko la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona busara ya kukutana na wadau hao pamoja na Serikali ili kupata taarifa kutoka kwa pande zote mbili ili Bunge kupitia Kamati kuweza kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali namna ya kutatua changamoto hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na wadau kwa wakati wake na baadae ikakutana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo ndiyo yenye dhamana ya Habari kwa maana ya Maudhui pamoja na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano (TCRA) ambao ndiyo

Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano kwa maana ya miundombinu ya Habari.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi suala hili ili.**

## **2.6 Uchambuzi wa Miswada na Mikataba ya Kimataifa (Maazimio)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki, Kamati ilichambua Muswada mmoja wa Sheria kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (7) b iliyo chini ya kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Muswada huo uliojulikana kama Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Ualimu Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Teacher's Professional Board Bill, 2018*) ulichambuliwa kwa takribani siku 5 zilizojumuishia kukutana na wadau.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania ulichambuliwa na Kamati katika vikao vya mwezi Agosti, 2018 kwa kufuata taratibu zote za ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa masuala ya taaluma ya ualimu ili kuisaidia Kamati katika kufanya

uchambuzi ulio makini ili kuweza kutunga sheria yenye tija. Baada ya uchambuzi wa Muswada, Kamati iliwasilisha taarifa ya Maoni na mapendekezo kuhusu Muswada huo mbele ya Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 5 Septemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuisitiza kuwa uwepo wa Sheria hii utasaidia kusimamia taaluma ya ualimu kwa weledi mkubwa na kuimarisha taaluma ya ualimu na kuipa heshima yake. **Ni maoni ya kamati kuwa Serikali itafanya jukumu lake la kuhakikisha Waziri mwenye dhamana anatunga Kanuni mbalimbali ili iweze kuanza kutumika kwa manufaa ya wenye taaluma ya ualimu pamoja na taifa zima kwa ujumla.**

## **2.7 Semina kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa majukumu ya Kamati unategemea ushirikiano wa Ofisi ya Bunge, Serikali na taasisi mbalimbali za Serikali na za Binafsi katika kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala mbalimbali ili waweze kutoa ushauri wa kujenga na wenye tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati, semina kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na Sekta ya Elimu, Afya na maendeleo ya Jamii pamoja na tasnia ya Habari zilitolewa na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee wakishirikiana na Mfuko wa Fedha wa Dunia (Global Fund), EngenderHealth, SIKIKA na TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya habari, Utamaduni, Sanaa na michezo, HAKI ELIMU , STIPTRO, Umoja wa wawekezaji wa shule binafsi Tanzania (Tanzania Private Investors in Education-TAPIE), Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa **Parliamentary Legislative Support Programme II (LSP II)**, Voluntary Service Overseas - VSO Tanzania) na Legal Service Facility.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawashukuru wadau wote kwa namna walivyoweza Kamati kutekeleza majukumu yake kutokana na elimu nzuri waliyoipata kupitia semina hizo.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

#### **3.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA utekelezaji wa majukumu ya Wizara zote kwa ajili ya kuwaletea watanzania maendeleo unategemea uwepo wa bajeti ya kutosha ya fedha zilizotengwa na Serikali na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Haitoshi uwepo wa bajeti pekee bali na upelekaji wa fedha hizo za bajeti katika Wizara husika kwa wakati ili kuwawezesha watendaji wa Wizara hizo kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka wa Fedha husika,

**NA KWA KUWA** bado mwenendo wa bajeti siyo wa kuridhisha hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inazidi kusesitiza Serikali iendelee kupeleka fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

### **3.2 Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA**, Katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 Serikali iliidhinishwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wizara tatu ambazo Kamati inazisimamia,

**NA KWAKUWA**, Katika Miradi yote ambayo Kamati ilifanya ukaguzi mwezi Machi, 2018, hakuna mradi hata mmoja ambao ulikuwa umepelekewa fedha. Baadhi ya miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ilikuwa inatumia bakaa za fedha za miaka iliyopita,

**KWA HIYO BASI** Kamati inaendelea kusesitiza kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuepusha kutekelezwa kwa hasara kutokana na kupanda kwa thamani ya fedha kulingana na tofauti za nyakati.



### **3.3 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Wizara hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

#### **3.3.1 Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI)**

##### **a) Kanzi data (Database) ya AZAKI zote**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** kwa mujibu wa taarifa za Wizara kuna zaidi ya AZAKI 8,000 nchini zilizojikita katika nyanja za afya, maendeleo ya jamii kwa maana ya watoto, wazee na hata masuala ya kijinsia hasa kwa wanawake,

**NA KWA KUWA** pamoja na AZAKI hizi kufanya shuguli zake katika maeneo mbalimbali ya nchi mijini na vijijini lakini Wizara kama wasimamizi wa AZAKI haina taarifa za uhakika wa wapi zilipo na hata wakati mwingine Wizara hazifahamu shughuli maalumu zinazotekelezwa na AZAKI hizo na kuifanya Serikali kushindwa kufuatilia utekelezaji wa shughuli zake,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Wizara kutengeneza kanzidata ambayo itaonesha jina la AZAKI, mahali

inapotekeleza majukumu yake, wafadhili wa fedha wa AZAKI husika, aina ya majukumu yanayotekelezwa. Kwa kufanya hivyo Wizara itakuwa imesaidia kufanya uratibu na usimamizi wa AZAKI zote nchini.

**b)Wizara ianzishe Kitengo cha Udhibiti ubora wa AZAKI**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** uanzishwaji wa AZAKI unafanyika kwa mujibu wa Sheria na miongozo yake lakini pia zinahitaji udhibiti wa ubora wa shughuli inazofanya,

**NA KWA KUWA** zipo asasi ambazo zinafanya vizuri na baadhi zinakwenda kinyume na sheria na miongozo ya Serikali hali ambayo inaleta ukakasi kwenye jamii,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Wizara kuanzisha kitengo cha udhibiti ubora wa AZAKI ili kuweza kuzisimamia na kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kuzichukulia hatua kali ikiwemo onyo na hata kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria ikithibitika zimekwenda kinyume na sheria za nchi. Kwa kufanya hivyo zitaongeza uwajibikaji na

usimamiaji wa sheria na miongozo ambayo Serikali imewekwa kwa maslahi mapana ya nchi na wananchi kwa ujumla.

### **3.3.2 Bajeti ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Utekelezaji wa majukumu ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii unategemea sana kiasi cha fedha kinachotengwa,

**NA KWA KUWA** kwa muda mrefu Idara hii haijawahi kutengewa zaidi ya shilingi **Bilioni 50** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo miradi ya Maendeleo, Kamati inaona ni kikwazo kikubwa katika utendaji wa majukumu ya Idara hiyo na ukizingatia kwamba Idara hii inabeba kundi kubwa la watoto, wazee na Jinsia zote (watanzania wote),

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ianze kubadili mtazamo wake na kuipa umuhimu Idara hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha ili iweze kutatua changamoto za Sekta mbalimbali, ikiwemo ya Kilimo, afya, maji, miundombinu,

utalii na nyingine kwa kuwa kila jambo linaanzia katika jamii kupitia maafisa Maendeleo ya Jamii walio katika kila kata hapa nchini ili kuweza kuwaletea maendeleo wananchi.

### **3.3.3Ukatili wa Kijinsia na Watoto**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeainisha kwamba nanukuu ***“Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria,”***

**NA KWA KUWA** hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia na watoto hususan katika Mkoa wa Njombe ambapo watoto wanaendelea kuuwawa jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya nchi yetu na matakwa ya makubaliano ya kimataifa lakini pia ni kinyume na haki za binaadamu,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Serikali ifanye uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo hivi vya kinyama.

### 3.3.4 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

#### a) Muswada wa Sheria ya Bima ya afya kwa wote

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** afya ni mtaji mkubwa katika kujiletea maendeleo kwa nchi husika na kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikishauriwa na kupokea mapendekezo ya Kamati kwamba ni wakati sasa umefika kukawepo na Bima ya Afya kwa watu wote (*Universal Health Coverage*) lakini inashindikana kwa kuwa hakuna Sheria ambayo itaweza kusimamia aina hiyo ya bima,

**NA KWA KUWA** Kamati inaona umuhimu mkubwa wa aina hii ya Bima kwa wananchi wote ambayo itaondoa ubaguzi wa nani awe na bima na nani asiwe nayo. Hali ilivyo sasa ni wale walio katika ajira rasmi tu ndiyo wanufaika kwa asilimia kubwa na Bima ya taifa ya afya ambao hawazidi asilimia 27 ya wataanzania wote,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuharakisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote (*Universal Health Coverage Bill*) ili

kuiwezesha NHIF kutekeleza jukumu la kutoa bima ya Afya kwa wananchi wote na kuwapa uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya.

**b) Maboresho ya Huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mfuko wa umma unaotoa huduma zake kwa wananchi hasa kwa watu ambao wapo katika ajira rasmi (Utumishi wa Umma) na sasa imepanua huduma zake kwa kuwaingiza wale ambao wapo katika sekta binafsi kwa maana ya kujiajiri na hata kuajiriwa na Sekta binafsi,

**NA KWA KUWA,** Licha ya kufanya hivyo bado wananchi wengi hawafahamu umuhimu wa kuwa na bima ya afya na namna gani kama mtu binafsi au vikundi wanaweza kupata huduma ya bima ya afya kutokana na kukosekana kwa baadhi ya mambo ikiwemo uhamasishaji mdogo wa jamii, vifurushi vichache au visivyovutia vinavyotolewa na bima ya afya ambavyo vinampa uwanja mdogo

mteja wa kuweza kuchagua nini anahitaji pamoja na gharama zake. Kamati inaona kuwa vifurushi vinavyopangwa vinatokana na maamuzi ya Mfuko wa Bima ya Afya wenyewe na siyo mahitaji ya wateja wake jambo linalopelekea wananchi kutoona umuhimu wake,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa:-

- i) Serikali kupitia NHIF iendelee kufanya uhamasishaji kwa wananchi kuhusu umuhimu wa Bima ya afya ili kuwawezesha kuwa na uhiari wa kujiunga na Bima ya afya kulingana na mahitaji yao kama vile uwezo wa kiuchumi (Social stratification), ambapo kuna baadhi ya wahitaji wanataka huduma ya kwenda kutibiwa nje ya nchi ili mradi akubaliane na gharama za ulipaji wa bima hiyo ambapo mashirika ya kimataifa na taasisi kama Benki ya Dunia watakuwa tayari kujiunga na Bima hii ili mteja apate kile anachohitaji. Aidha, NHIF iwe inafanya utafiti mara kwa mara na kuona ubadilikaji wa mahitaji ya wateja kutokana na

maoni yao ili kuweza kutengeneza vifurushi vinavyoendana na mahitaji ya wateja hao; na

**ii)** NHIF ifanye mchakato wa kutafuta wateja badala ya kusubiri kuletewa wateja kwa mujibu wa sheria kama ilivyokuwa awali kwamba watumishi wa Umma wote ni wateja wao na sasa wameongezewa mashirika na taasisi zote za umma ambazo zilikuwa zinapata huduma ya bima ya afya kutoka kwa watoa huduma wengine, hali hii isipelekee kushindwa kufanya shughuli za kutafuta wateja wengine.

**c) Tathmini (Actuarial Valuation) ya Mfuko wa Taifa Bima ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mfuko wa wananchi ambao wanahudumiana kwa kuchangishana (*Risk Pooling Strategy*) kila mwezi ili kuweza kupata huduma za afya kwa maana ya kwamba anayeugua anahudumiwa na walio wazima. Fedha hizi



zinapaswa kuwepo na mteja aone kama zipo anatarajia kupata huduma za afya wakati wowote na mahali popote alipo bila kikwazo chochote cha kutokuwepo kwa dawa, mtoa huduma ya afya, vifaa tiba kwa maana ya kupata vipimo ili kutambua ugonjwa unaomsumbua na masuala mengine yanayoendana na hayo,

**NA KWA KUWA** Kamati imekuwa ikishuhudia Mfuko huu ukifanya uwekezaji wa aina mbalimbali na hata kutoa mikopo kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya kufanya uwekezaji ambao baadhi haiendani na hata na masuala ya afya hali ambayo inaweza kupelekea Mfuko kutofanya majukumu yake ya msingi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa, Mfuko huo utekeleze majukumu yake ya msingi ambayo ni malengo mahsusi ya kuundwa kwake. Aidha, Serikali ifanye tathmini ya mfuko (*Actuarial Valuation*) huo ili kuweza kufahamu uhai na nguvu ya Mfuko baada ya kufanya uwekezaji huo mkubwa kwa nyakati

tofauti. Kwa kufanya hivyo, Serikali itafahamu changamoto zake na namna gani ya kuweza kuzikabili kisha kuona namna bora ya kuendelea kuuimarisha Mfuko kwa manufaa wa wanachama wake.

### **3.3.5 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

#### **a) Serikali kutolipa deni la MSD kwa wakati;**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Bohari Kuu ya Dawa ndiyo yenye jukumu la kununua na kusambaza dawa hapa nchini na imekuwa ikitekeleza majukumu yake katika mazingira magumu sana licha ya kuwa Serikali imeongeza fedha za dawa katika Wizara ya Afya na kuendelea kudaiwa kiasi cha Zaidi ya Bilioni 200. Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikitoa huduma hiyo licha ya Serikali kutolipa madeni hayo kwa wakati huku ikiendelea kutaka kupatiwa huduma. Hali hii inafanya Bohari kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Maelezo ya Serikali ni kwamba bado inahakiki deni hili,

**NA KWA KUWA** MSD imeongeza wigo wa utekelezaji wa majukumu yake hadi kwa nchi nyingine licha ya

kwamba haitatumia fedha za Serikali kusambaza dawa hizo katika nchi jirani lakini bado zitatumika katika kuwawezesha watendaji kusimamia majukumu hayo yaliyoongezeka,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kwamba fedha zilizotengwa kiasi cha shilingi Bilioni 50 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kikatolewa haraka wakati uhakiki huo ukiwa unaendelea kwani kwa vyovyote vile deni halitapungua kiasi hicho cha shilingi Bilioni 50. Aidha, mpaka Septemba 2018 deni la Serikali lilikuwa limefikia kiasi cha Shilingi Bilioni 200 ingawa Taarifa imeonesha ni shilingi Bilioni 114 nalo lipo katika uhakiki.

**b)Mkakati wa kuwawezesha wawekezaji katika uzalishaji wa dawa hapa nchini**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** nchi yetu ina kauli mbiu ya Uchumi wa Viwanda na moja ya eneo ambalo Serikali inaweza ikafanya vizuri sana ni katika uwekaji wa mazingira bora ya viwanda vya uzalishaji wa dawa za binadamu hapa nchini,

**NA KWA KUWA** ili kufanikiwa katika uzalishaji wa dawa hapa nchini, ushirikishwaji wa Sekta binafsi ni muhimu ili ziweze kuzalisha dawa hizo hapa nchini kwa gharama nafuu,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa mpango wa kuziwezesha sekta binafsi katika kuzalisha dawa hapa nchini ili kuendelea kupunguza gharama za dawa kama ilivyo sasa. Kwa kufanya hivi, Serikali itakuwa imetimiza Sera yake ya Uchumi wa Viwanda, itapunguza gharama zinzotumiwa na MSD katika manunuzi ya dawa nje ya nchi kwa gharama kubwa lakini pia katika kuwawezesha wawekezaji na wananchi katika kupata dawa za uhakika hapa nchini.

### **3.3.6 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mamlaka ya chakula na Dawa ndiyo yenye jukumu la kuhakikisha usalama wa mlaji wa chakula, vipodozi pamoja na dawa nchini,

**NA KWA KUWA**, katika vikao vya Kamati, iliwasilishwa taarifa ya kuwepo kwa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu zikiwemo chakula, dawa na vipodozi hali iliyopekea mamlaka kiviteteza ambavyo vilikuwa na jumla ya uzito wa **tani 453.6** zenye thamani ya shilingi **6,940,348,743**. Bidhaa hizi ni pamoja na zile zilizokwisha muda wake na kutolewa taarifa na wateja wenyewe, zinazothibitika kuwa ni duni na bandia baada ya uchunguzi wa kimaabara au bidhaa zinazokutwa katika maeneo ambayo hayajasajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kutengeneza Alama maalum ya utambuzi wa ubora wa bidhaa (*Barcode*) itakayomilikiwa na Mamlaka kama ambavyo ilivyo kwa Shirika la viwango Tanzania (TBS) wanayo alama ya utambuzi wa ubora wa bidhaa. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza matumizi ya vyakula, dawa na hata vipodozi ambavyo havina uhakiki wa mamlaka ya Chakula na Dawa.

### **3.3.7 Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Sera ya Afya inaelekeza huduma za afya kwa watoto, wajawazito na wazee wa kuanzia miaka sitini (60) kupewa huduma hizo bila malipo,

**NA KWA KUWA,** Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ni miongoni mwa Taasisi inayotoa huduma hizo kwa makundi maalumu bila malipo na kupelekea taasisi kuingia gharama kubwa ya shilingi **607,444,779.93** kwa kipindi cha nusu mwaka (Juni-Disemba, 2018) kuweza kufidia gharama hizo hali inayoipelekea Taasisi kushindwa kujiendesha vizuri,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kutoa ruzuku kwa taasisi hii na taasisi za Afya zote nchini kwa ajili ya kufidia gharama za matibabu kwa makundi maalumu yaliyotajwa ili kuzisaidia kuendelea kutekeleza huduma zake za kutoa huduma za afya.

### **3.4 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

#### **3.4.1 Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

##### **a) Kuongeza idadi ya Wakalimani**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo inatambulika kitaifa na kimataifa, ambapo hata nchi jirani kama Rwanda zimerasimisha lugha hii kutumika kama lugha ya mawasiliano ndani ya nchi hiyo,

**NA KWA KUWA** lugha hii imeanza kutumika katika mikutano mikubwa ya ndani na nje ya nchi ya Tanzania lakini kuna changamoto ya wakalimani kwani wakalimani waliopo wanaojua lugha mbalimbali hawazidi 10 idadi ambayo ni ndogo sana ikilinganishwa na uhitaji wake,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri ili lugha hii iweze kutambulika Kimataifa ni vyema Serikali ikaweka mkakati madhubuti wa kuongeza idadi ya Wakalimani ili waweze kuzitumia fursa zilizopo. Aidha, mkakati huo ujielekeze pia katika kuhakikisha

wakalimani hawa wanakuwa na uelewa wa lugha nyingi zaidi kama vile Kifaransa, Kireno, Kijerumani na hata Kichina.

**b) Tuzo ya Kiswahili**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali ina mikakati mbalimbali ya kukuza lugha ya Kiswahili ikiwemo kuheshimu michango ya watu/nchi mbalimbali katika kuikuza lugha hiyo kwa kuwapa Tuzo ya Kiswahili ijulikanayo “Tuzo ya Shaban Robert”,

**NA KWA KUWA** baadhi ya watu/nchi kama vile Afrika ya kusini na Rwanda zimekuwa mstari wa mbele kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi zao,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza watu/nchi hizo na nyingine zitambuliwe na kupewa Tuzo ya Shaban Robert, kwa kufanya hivi kutaifanya lugha ya Kiswahili kuendelea kutangazwa na kutambulika kote ulimwenguni.



### **3.4.2 Sheria ya Huduma za Habari**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mwaka 2016 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Huduma za Habari (The Media Services Act, 2016) kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya Habari ikiwemo weledi wa wanataaluma ya uandishi wa Habari, wamiliki wa vyombo vya habari ikiwemo magazeti, redio na Televisheni,

**NA KWA KUWA,** Kamati imekuwa ikishuhudia baadhi ya magazeti yakikiuka maadili, taaluma na weledi wa kupasha habari hapa nchini,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali isimamie kikamilifu Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 kwa kuvichukulia hatua vyombo vyote vya habari, wamiliki wake wanaokiuka Sheria kama ambavyo ilikusudiwa uundwaji wake ili kuweza kuitunza heshima ya nchi yetu.

### 3.4.3 Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)

#### a) Uibuaji wa vipaji mbalimbali vya wasanii katika jamii

**KWA KUWA** kuna vipaji vingi ambavyo vipo kwenye jamii lakini Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) halijaweza kuvitambua,

**NA KWAKUWA** kuibuliwa kwa vipaji hivyo kutaongeza idadi ya wasanii waliopo nchini na hivyo kuongeza mapato ya nchi kutokana na kazi watazokuwa wanafanya,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kupitia BASATA iandae mkakati maalumu wa kuibua vipaji hivyo kuanzia ngazi ya chini ya jamii ili kuweza kuwa na wasanii wengi ambao kwa namna moja ama nyingine wataendelea kuipeperusha bendera ya Tanzania, ikumbukwe sanaa ni ajira.

#### b) Wasanii

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** moja ya kazi za BASATA ni kutoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa Sanaa nchini na hivi karibuni kumekuwa na

fungia fungia ya nyimbo za wasanii na matamasha ya wasanii,

**NA KWA KUWA** wasanii hawa wamekuwa wakipata mapato mengi kutoka na HITS wanazopata kupitia mitandao ya jamii kama Youtube na Serikali imekuwa haipati chochote kutokana na mahusiano yasiyoridhisha kati yao na wasanii,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza;

- i) BASATA kutekeleza jukumu la kuwalea kwa kuwashauri wasanii kuandaa nyimbo zinazoendana na maudhui na kuwaonya pale wanapokosea;
- ii) Kuboresha mahusiano na wasanii ili kuweza kufaidika na mapato yatokanayo na hits za mitandao ya jamii; na
- iii) BASATA kuhakikisha wanaandaa kanzidata (*Database*) ya kuwafahamu wateja wao (Wasanii wote) nchi nzima kwa kuwa na aina maalumu ya utambuzi (*Special Identification*)

ikiainisha jina, aina ya kazi anazozifanya na masuala mengine yanayoambatana na hayo. Hili linawezekana kwa kuwatumia maafisa utamaduni wa Wilaya, Mkoa na mwisho Baraza la Sanaa la Taifa.

### **3.4.4TASUBA**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** TASUBA licha ya kuwa ni Kituo cha Ubora uliotukuka (Centre of Excellency) lakini bajeti inayotengwa hususani fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Taasisi hii pamoja na miundombinu iliyopo haviendani na hadhi yake,

**NA KWA KUWA** pamoja na kufanya Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni lakini matangazo hayakuwa mengi kutokana na ukosefu wa fedha na hivyo kuathiri idadi ya washiriki pamoja na mapato,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri: -

- a) Bajeti ya TASUBA iongezwe hususan ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ikiwemo Miundombinu, na vifaa ili iweze kuboreshwa; na

b) TASUBA ianze kujitangaza hasa inapokuwa na matamasha ili yafanane na yale ya Sauti za Busara au Tamasha la Kimataifa la Filamu Zanzibar (ZIFF) kwani itasaidia kupata washiriki wengi na mapato ya Serikali kuongezeka.

### **3.4.5 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

#### **a) Chaneli ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** TBC imeanzisha chaneli ya Utalii kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii, maliasili, mali kale na utamaduni wa Mtanzania ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi,

**NA KWA KUWA** Chaneli hii bado inaonekana ndani ya nchi pekee licha ya mpango wa TBC kutaka ionekane hadi nje ya nchi ili kuweza kuvutia watalii wa nje ya nchi na hivyo kuongeza pato la Taifa,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri TBC kuandaa mpango mkakati ambao utahakikisha chaneli hii

inaonekana nje ya nchi mapema ili kuwavutia watalii wengi na hatimae kuongeza pato la Taifa kutokana na ujio wao.

## **b) Mapato ya TBC**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** ili TBC iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama zilivyo Televisheni nyingine za Umma katika nchi mbalimbali duniani inahitaji kuwa na uwezo wa kifedha,

**NA KWA KUWA** kwa muda mrefu sasa TBC inashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kutokana na ufinyu wa fedha ili hali kuna uwezekano wa kutumia vyanzo vingine vya mapato kama vile tozo za ving'amuzi na ada za leseni za Televisheni nyingine,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu utakaowezesha TBC kupata sehemu ya mapato yatokanayo na malipo ya muda wa hewani wa visimbuzi pamoja na ada za leseni za Televisheni nyingine ili kuiwezesha kifedha katika utekelezaji wa majukumu ya Umma.

### **3.4.6 Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF)**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ndiyo yenye jukumu la kusimamia mchezo wa mpira wa miguu nchini,

**NA KWA KUWA**, kumekuwa na changamoto nyingi katika usimamizi na uratibu wa mpira wa miguu nchini,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri

- a) Wizara yenye dhamana na Michezo ishirikiane na TFF kuhakikisha kuwa hakuna mabadiliko ya mara kwa mara ya ratiba za Ligi Kuu ili kuondoa dhana ya upangaji wa matokeo;
- b) Wizara ishirikiane na TFF kuondoa migogoro katika vilabu na vyama vya michezo;
- c) Serikali iandae program za mafunzo kwa makocha wa mpira wa ndani ili kuinua soka letu; na
- d) Serikali iachane na ratiba za michezo ya ligi ya wanawake inayochezwa nyumbani na ugenini

na badala yake ichezwe kwenye vituo ili kupunguza gharama kwani timu nyingi hazina uwezo.

### **3.5 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

#### **3.5.1 Mkakati wa kuboresha miundombinu ya Vyuu**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wa chuo kikuu unategemea na uwepo wa Miundombinu bora inayotosheleza kama Mabweni ya wanafunzi yenye huduma zote ikiwemo maji safi na salama, Ofisi za Wahadhiri, Maabara, maktaba vikianishwa kwa uchache,

**NA KWA KUWA** kumekuwa na changamoto ikiwemo upungufu wa baadhi ya miundombinu kama vile mabweni katika baadhi ya vyuo mfano Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hali inayoathiri utekelezaji mzuri wa majukumu ya chuo na usalama kwa wanafunzi hasa kwa watoto wa kike,



**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iandae mkakati wa maksudi na wa haraka, ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wanaokaa nje ya chuo kwa maana ya **Off - Campus** kwenye nyumba za watu binafsi. Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itafanya juhudi hizo za maksudi kama ambavyo ilifanyika kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salama kwa kujenga mabweni ya wanafunzi hali ambayo imemaliza kabisa changamoto ya wanafunzi kukaa nje ya chuo.

### **3.5.2 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl J.K Nyerere kiendane na jina**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndiye muasisi wa Taifa linaloitwa Tanzania leo, ndiye Rais wa kwanza wa nchi ya Tanzania, ndiye aliyeongoza harakati za kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni waliotutawala katika Nyanja zote za kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na hata kifikra, ndiye aliyeifanya nchi hii ikatambulika ndani na nje ya Bara la Afrika. Si hivyo tu, jina lake pia linatambulika nje ya nchi kwa mchango wake katika kujipatia uhuru na hata usuluhishi wa migogoro mbalimbali katika nchi nyingine duniani,

**NA KWA KUWA**, kutokana na sifa chache zilizotajwa hapo awali, Serikali iliona umuhimu wa kumuenzi Baba wa Taifa kwa kutoa jina na kukiita Chuo kilichopo Kigamboni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambacho wakati Kamati ikipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake ilibaini kwamba jina ambalo Chuo limepewa (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere) ni kubwa na haliendani na shughuli ambazo Chuo inatekeleza,

**KWA HIYO BASI**, ili kutunza hadhi ya jina la mwalimu na hata kuweza kutambulika katika nchi nyingine na kuwafanya watu kutoka nchi hizo kutamani kuja Tanzania na kusoma katika Chuo chenye jina la muasisi wa Taifa na ili kuondoa hali ilivyo kwa sasa, kwamba wanafunzi wanaokosa sifa za kujiunga na vyuo vingine hapa nchini ndiyo wanaokwenda kujiunga na masomo katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambayo Kamati inaona si sawa hata kidogo. Kamati inashauri: -

a) Chuo kijielekeze katika kutoa mafunzo ya uongozi ili iweze kuwa “*Centre of Excellency*”. Hii itasadia kuvutia

watu wengi kujiunga na chuo lakini wahadhiri wengi bora wenye kufundisha masuala ya uongozi kwenda kufundisha katika Chuo hicho na kuondokana na changamoto ya upungufu wa watumishi; na

b) Chuo kianzishie mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na yatolewe kwa viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya kijiji mpaka Taifa ili waweze kufahamu kwa kina misingi ya uongozi bora na uzalendo.

### **3.5.3Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

#### **a) Vigezo vya upatikanaji wa Mkopo**

**Mheshimiwa Spika, KWAKUWA,** Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kusomesha wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu zaidi ya kiasi cha shilingi **Bilioni 400** kila mwaka kwa njia ya kuwapa mikopo ambayo inapaswa kurejeshwa na wafaidika hao mara wamalizapo masomo,

**NA KWAKUWA,** Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ndiyo inayosimamia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vilivyoainishwa

na Bodi ikiwemo hali ya uchumi, historia ya shule mwanafunzi alizosoma ikiwemo sekondari, hali ya wazazi (*death status*) vikitajwa wa uchache wake ambavyo Kamati inaona ni vichache,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuvipitia tena vigezo hivyo na ikibidi kuboreshwa na kuongezwa kwa vigezo vingine kama vile ufaulu wa mwanafunzi bila ya kujali hali ya uchumi wa familia, jinsi ya kike lakini pia kwa wanafunzi wenye ulemavu na wana ufaulu mzuri wapewe mkopo bila kuangalia vigezo vingine ikiwemo historia yake.

**b) Mwenendo wa Ukusanyaji wa madeni ya Mikopo kutoka kwa wanufaika**

**KWAKUWA**, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa muda mrefu tangu mwaka 1994/1995 mpaka Desemba 2018 jumla ya shilingi **Trilioni 3.87** kwa **wanufaika 478,548** zimetolewa,

**NA KWA KUWA**, katika kiasi kilichotolewa (Trilioni 3.87) na Serikali kwa wanufaika mbalimbali ni takribani shilingi

**Bilioni 291.538** bado hazijarejeshwa ambazo ni sawa na **asilimia 70** ya bajeti ya fedha (**Bilioni 412.4**) ya Bodi ya mikopo kwa wanufaika kwa mwaka **2018/2019** zipo mikononi mwa wanufaika zinapaswa kurejeshwa kwa Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wengine kwani wahitaji wanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali yafuatayo;

- i) Bodi ya mikopo iimarishe mifumo ya taarifa za wanufaika wa mikopo kwani kumekuwepo na malalamiko ya baadhi ya wanufaika kudaiwa deni zaidi ya mara moja ili hali mtu huyo ameanza kurejesha au amemaliza malipo ya mkopo;
- ii) Kuandaa utaratibu rahisi na wa kisasa kwa wanufaika kuweza kupata taarifa za deni lake na kuweza kulipa kupitia mfumo wa simu za mkononi kwa kuwa wanufaika wengi wanao uwezo wa kumiliki simu za mkononi, kwa kufanya hivyo kutarahisisha ukusanyaji wa madeni hayo; na

iii) Bodi ya Mikopo iandae orodha ya wadaiwa wote wanaostahili kulipa madeni (madeni yaliyoiva Bilioni 291.538) hayo na kuyasambaza kwa waajiri, taasisi mbalimbali na kwenye vyombo vya habari ili kuweza kuwahamasisha na kuwakumbusha wadaiwa hao kuweza kulipa madeni hayo ya mkopo.

### **3.5.4 Miradi ya Lipa kulingana na Matokeo (EP4R) kusimamiwa na Wizara ya ELIMU**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mradi wa EP4R umekuwa na tija chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kamati imeshuhudia uwepo wa thamani ya fedha katika maeneo yote ambayo mradi umekuwa ukitekelezwa,

**NA KWA KUWA,** hivi karibuni kumekuwa na minong'ono ya kutaka Mradi huu uanze kusimamiwa na watendaji wa TAMISEMI jambo ambalo Kamati inaona si jema kwa kuwa TAMISEMI inashughuli nyingi za kufanya zikiwemo barabara, maji, elimu na afya,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaendelea kusesitiza Miradi yote inayohusu uboreshaji wa miundombinu ya elimu chini ya EP4R iendeleo kutekelezwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

### **3.5.5 Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** malengo ya chuo kikuu cha Dodoma ni kudahiri **wanafunzi 40,000**,

**NA KWA KUWA**, Mpaka kufikia mwaka 2018/2019 Chuo kimedahiri jumla ya **wanafunzi 28,776** kutokana na changamoto ya fedha za miradi ya maendeleo zikiwemo za ukamilishaji wa ujenzi wa chuo lakini pia kutokana na uhaba wa wafanyakazi hasa wanataaluma katika ngazi za madaktari na maprofesa wa kufundisha wanafunzi hao,

**KWAHIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ikipatie chuo fedha hizo za miradi ya maendeleo ili kikamilishe ujenzi wa chuo utakaowezesha udahiri wa wanafunzi wengi zaidi lakini pia iweke mkakati madhubuti utakaohakikisha chuo kinakuwa na walimu wa kutosha wa kufundisha lengo la wanafunzi hao 40,000.

### **3.5.6 Vyuvo vya Ufundi**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** Serikali ya awamu ya Tano imejikita katika kukuza uchumi wa viwanda na kuipeleka nchi katika uchumi wa viwanda katika sekta mbalimbali ikiwemo viwanda vinavyohitaji ufundi wa aina tofauti tofauti kwa manufaa ya nchi yetu,

**NA KWA KUWA,** idadi ya mafundi mchundo na mafundi sadifu wanaozalishwa na vyuo vya ufundi nchini ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango mkakati wenye tija na wa muda mrefu wa kuimarisha vyuo vya ufundi kwa kuongeza miundombinu bora, walimu wa kutosha na ikiwezekana kuwapa mikopo wanafunzi hao kama ambavyo wanafunzi wa elimu ya juu wanapata kwa ajili kuzalisha mafundi mchundo na mafundi sadifu wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza Sera ya Viwanda na kuimarisha uchumi wa viwanda kwa maslahi mapana ya Taifa.



### 3.5.7 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

#### a) Asilimia 1 ya Pato la Taifa (GDP) kwenda COSTECH

**KWAKUWA**, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilianzishwa kwa lengo la kuwa Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohusiana na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa maendeleo ya Taifa zima,

**NA KWA KUWA**, Taarifa ya tume inaonesha kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini ambapo katika uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa Tume hii ilipaswa kupokea fedha kutoka Serikalini kiasi cha **asilimia moja** ya Pato zima la Taifa (1% of GDP) yakiwa ni makubaliano ya Nchi zote za Umoja wa Afrika (*African Union*) kwa lengo la kusaidia utafiti jambo ambalo limekuwa halifanyiki kwani upatikanaji wa fedha umekuwa ni **asilimia 0.034** ya Pato la Taifa kwa muda mrefu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza makubaliano yaliyofanywa na Umoja wa nchi za Afrika

za kutenga **asilimia 1** ya Pato la Taifa kwa mwaka ili kwanza kutimiza makubaliano ya nchi za Umoja wa nchi za Afrika lakini pia kuisaidia Tume kutekeleza majukumu yake ya utafiti.

**b) Fedha za Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (Telecommunication Traffic Monitoring System – TTMS)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** moja ya chanzo cha mapato ya Tume ni fedha za Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (*Telecommunication Traffic Monitoring System – TTMS*),

**NA KWAKUWA**, chanzo hicho cha mapato kwa sasa kimeondolewa hali inayopelekea utekelezaji wa majukumu ya Tume kuwa mgumu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuona namna bora ya kurudisha chanzo hiki cha mapato kwa Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

#### 4.1 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja nawe napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mawaziri wote 3 na Manaibu Waziri 3 ambao tunafanya kazi nao kwa karibu kwa ushirikiano mkubwa, nasema asante sana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummu Mwalimu (Mb), Naibu Waziri Dkt. Faustine Ndugulile (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Juliana D. Shonza (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) na Naibu Mhe. William T. Ole Nasha (Mb) wamekuwa karibu na Kamati na kuelewa Kamati inapotoa hoja za msingi katika kuendelea kuboresha utendaji mzuri wa Serikali. Aidha,

napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara hizo wakiongozwa na Makatibu Wakuu wao kwa utendaji mzuri wa kazi zao licha ya changamoto nyingi wanazokumbana nazo lakini bado wameendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Juma S. Nkamia, Mb kwa ushirikiano anaonipa mimi binafsi pamoja na Kamati katika kutekeleza majukumu yetu. Kipekee naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinionesha katika kutekeleza majukumu yangu lakini pia kutoa michango yenye tija kwa Taifa.

Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

- |                                    |              |
|------------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb     | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb   | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb   | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb  | Mjumbe       |
| 5. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali  | Mjumbe       |
| 6. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | Mjumbe       |

7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb Mjumbe
8. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb Mjumbe
9. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb Mjumbe
10. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb Mjumbe
11. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb Mjumbe
12. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb Mjumbe
13. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb Mjumbe
14. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb Mjumbe
15. Mhe. John Peter Kadutu, Mb Mjumbe
16. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb Mjumbe
17. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb Mjumbe
18. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb Mjumbe
19. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb Mjumbe
20. Mhe. Selemani Said Bungara, Mb Mjumbe
21. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb Mjumbe
22. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb Mjumbe
23. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb Mjumbe
24. Mhe. Maulid Said Mtulia, Mb Mjumbe
25. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kipekee zaidi napenda kumshukuru  
Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha

Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Nawashukuru pia wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge akiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati hii Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela E. Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati.

## **4.2 HOJA**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha Taarifa hii, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA  
JAMII**

**7 Februari, 2019**